HOTUBA YA WAZIRI WA MADINI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (MB) WAKATI AKIFUNGUA WARSHA YA SIKU MBILI YA KUJADILI KANUNI ZA UANZISHWAJI MASOKO YA MADINI NCHINI TAREHE 11 FEBRUARI, 2019 – JIJINI MWANZA

Mhe. John Mongela, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza

Prof. Simon Msanjila, Katibu Mkuu Wizara ya Madini

Mhandisi David Mulabwa, Kamishina wa Madini

Profesa Joseph Semboja, Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya UONGOZI

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya

Makatibu Tawala wa Wilaya

Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya

Mabibi na Mabwana.

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tujadili na kufahamishana maudhui, malengo na mtazamo juu ya uanzishwaji masoko ya madini nchini.

Napenda kuwashukuru sana Taasisi ya UONGOZI (UONGOZI Institute) kwa kukubali ombi la wizara yangu la kuandaa warsha hii muhimu japokuwa ombi lilitumwa ndani ya muda mfupi sana. Pili, naomba niwashukuru viongozi wote Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri mliohudhuria kwa kuitikia mwaliko ndani ya muda mfupi sana. Natambua ratiba za majukumu yenu zilivyo na mambo mengi lakini, hii imeonyesha ni kiasi gani sisi kama viongozi tunaelewa

mwelekeo wa Serikali ya awamu ya Tano juu ya usimamiaji wa rasilimali madini nchini.

Ndugu viongozi,

Warsha hii ni muhimu kwa Wizara ninayoisimamia ya Madini na nchi kwa ujumla kwa kuwa lengo kuu tulilojiwekea kama Wizara kwa sasa ni kuhakikisha mchango wa sekta hii kwenye uchumi na maisha ya wananchi unaongezeka zaidi. Lakini pia, ni kwa sababu Wizara inatambua kwamba ili mchango wa sekta ya madini uongezeke, ni muhimu viongozi katika ngazi zote za Serikali wakashiriki katika kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali inayowekwa na Wizara.

Napenda kuwajulisha viongozi wenzangu kwamba, Wizara teyari imeshafanya kikao na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa wiki chache zilizopita, na lengo la kikao kile lilikuwa ni kujenga uelewa wa pamoja juu ya maudhui ya kanuni za uanzishwaji masoko ya madini nchini. Kwa hivyo, tukio hili la kukutana na nyinyi viongozi wa Wilaya na Halmashauri ni kubwa na muhimu sana kwa nchi kwani baada ya hapa nina imani mtaondoka na kwenda kuanza kuandaa mazingira yatakayowezesha uanzishwaji wa masoko ya madini. Pia, nina imani kupitia warsha hii tutaweza kujifunza mambo mengine mapya ambayo yatatusaidia katika kuisimamia sekta hii.

Ndugu viongozi,

Najua mmeshaanza kukutana na maswali mengi kutoka kwenye jamii mnayoitumikia kuhusu masoko haya ya madini, namna yatakavyoendeshwa, wahusika ni kina nani na kama kweli yatasaidia kujibu changamoto zilizopo kwenye sekta ya Madini.

Kabla sijaelezea maeneo hayo matatu, naomba nieleze kwa ufupi historia ya mchakato wa uanzishwaji masoko ya madini nchini. Mwaka jana mwaka 2018, Wizara iliunda kamati maalumu chini ya Naibu Waziri wa Madini Mhe. Stanslaus Nyongo (MB)

iliyopewa kazi ya kubaini kwanini madini (hasa dhahabu na vito) yanatoroshwa nchini, hasa na wachimbaji wadogo.

Kamati hiyo iliainisha sababu nyingi tu zinazochangia utoroshwaji madini nchini. Lakini kwa asilimia kubwa Wachimbaji wadogo na wadau wanaonunua na kuuza madini, hasa ya dhahabu na vito, walisema ukosekanaji wa Masoko na mlolongo wa kodi na tozo ndio vyanzo vikuu vinavyosababisha utoroshwaji madini.

Wadau hao waliokutana na Kamati ya Naibu Waziri, walitoa ushirikiano mkubwa kiasi cha kuionyesha kamati njia mbalimbali zinazotumiwa kutorosha madini. Hivyo basi Kamati ilipendekeza kwamba mchakato wa kuanzisha masoko ufanyike haraka, na pia ilishauriwa kuangalia uwezekano wa kuzifuta kodi na tozo mbalimbali zilizokua zinalalamikiwa hasa na wachimbaji wadogo na wanunuzi wa madini yaani *dealers* na *brokers*.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wizara ilianza kuchukua hatua za haraka ili kufanikisha mchakato wa uanzishwaji masoko, lakini pia kuhusu mchakato wa kuziondoa kodi na tozo kwa wachimbaji wadogo uko hatua za mwisho na ndani ya muda mfupi ujao, zitafutwa. Tuna imani kwamba hatua hizi zitaweza kuziba mianya ya utoroshaji madini na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Serikali na kuleta tija kwenye maisha ya wananchi wetu.

Ndugu viongozi,

Mchakato unaoendelea wa kuandaa kanuni hizi za Masoko ya Madini umezingatia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujifunza kutoka nchi mbalimbali ambazo zina masoko ya madini, lakini pia umezingatia mazingira ya kisheria kupitia kifungu cha 27(C) cha sheria ya Madini, 2010. Hivyo basi, niwaombe ndugu viongozi tusikilize kwa kina na kujadili mada

muhimu kuhusu suala hili ili kama kuna mapungufu, basi mtupatie ushauri na sisi kama Wizara tutaufanyia kazi.

Pia niseme tu kwa ufupi kwamba, kanuni hizi zinatoa nafasi kwa mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa kutengeneza mazingira wezeshi na pia zinatoa nafasi ya kushiriki katika kuyasimamia masoko hayo. Lakini pia, uzoefu wa nchi zingine umeonyesha kwamba masoko hayawezi kuanzishwa kwenye kila Wilaya au Mkoa, bali hutegemea upatikanaji wa madini kwa ajili ya masoko na vitu vingine kadhaa. Hivyo, hata kama masoko hayataanzishwa kwenye kila Wilaya na Halmashauri, kama viongozi wa ngazi hizo mna wajibu wa kuhakikisha kwamba madini yatakayozalishwa katika maeneo yenu yanapelekwa katika masoko yatakayoanzishwa ili yawe endelevu.

Nishauri tu kwamba, kati ngazi zetu za Wilaya na Halmashauri, tuna wajibu wa kuendelea kuwajenga, kuwalea na kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa sababu mazao yao ndio tunategemea yatauzwa katika masoko haya.

Kwa muktadha huo, ni matumaini yangu kwamba, Warsha hii inatuweka pamoja kama wasimamizi wakuu wa sekta na itatukumbusha tu kwamba majukumu ya usimamizi wa sekta ya madini, sio ya Wizara pekee na walo sio ya Maafisa Madini wakazi, bali ni yetu sote kwa ngazi tulizopo.

Ndugu viongozi,

Niseme tu kwamba, Warsha hii inafanyika katika kipindi muafaka kabisa, kipindi ambacho kumekuwepo na upotoshwaji wa taarifa zinazohusu sekta yetu ya madini. Hivyo viongozi wenzangu, kipindi hiki ni rahisi sana kutokea upotoshaji na pia kuongezeka kwa matarajio (high expectations) kwa wananchi kuhusu faida na hasara za masoko ya madini.

Njia pekee ya kujibu na kutolea ufafanuzi taarifa zitakazokuwa za kupotosha, ni kutumia maelekezo yaliyopo kisheria kupitia sheria ya Madini ya 2010 na sheria nyingine mtambuka.

Hivyo basi nisisitize tu tena kwamba, ni vizuri tukazielewa vizuri kanuni hizi zitakazowasilishwa na sheria ya Madini kwa ujumla, ili iwe rahisi kuzielezea kwa wananchi na wadau wa madini.

Ndugu viongozi,

Mimi binafsi kama mkazi na mzaliwa wa maeneo yenye uchimbaji madini, nisingependa hata siku moja kuona tunafarakana kama Taifa, kisa kugombania utajiri wetu kwa sababu watakaofaidika na mifarakano yetu ni wengine. Nisingependa kuona tunajuta kuwa na rasilimali hizi kutokana na kuhatarishwa kwa amani, utulivu, usalama na hata uhai wetu kwa ujumla. Ningependa kuona Madini yetu yanakuwa kiungo bora katika harakati za kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Pamoja na changamoto zilizopo katika usimamizi wa sekta hii nchini mwetu, namshukuru Mungu kwani rasilimali hizi hapa nchini hazijageuka kuwa balaa *(curse)* na ninaomba kwa Mungu hilo lisitokee. Naamini tukifanya mambo yafuatayo, hatutakuwa na tatizo kabisa katika usimamizi wa rasilimali hizi:

1. Kutoa taarifa zote muhimu za mapato yatokanayo na uchimbaji madini kwa wananchi ili wajue nini kinaendelea na waone manufaa ya uwepo wa madini katika maeneo yao;
2. Kuwashirikisha wananchi katika ngazi zote za maamuzi na kutekeleza mipango ya maendeleo inayotokana na shughuli za madini;
3. Kuwekeza mapato yatokanyo na shughuli za madini kwenye miradi endelevu hasa miundombinu na elimu (tangible/physical investments); na
4. Kutoa elimu kwa wadau wote kuhusiana na mnyororo wa thamani (value chain) wa usimamizi wa rasilimali hizi asilia.

Ndugu viongozi,

Nirudie kusema kuwa nimefarijika sana, tena sana kwa mwitikio wenu na pia niwashukuru watendaji wa Wizara yangu na Taasisi ya UONGOZI kwa kuandaa mkutano huu ndani ya muda mfupi sana ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu kanuni hizi zinazotoa msingi wa kisheria wa kuanzisha masoko ya madini. Ni matumaini yangu kwamba Taasisi ya UONGOZI na wadau wengine mtaendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili tuweze kufikia malengo mapana tuliyojiwekea.

Kwa upande wenu Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Makatibu Tawala, ni matumaini yangu kwamba kila mmoja wenu atajifunza kitu kutoka kwenye warsha hii, ambacho kitamsaidia katika utendaji wake wa kazi na hasa katika kutekeleza majukumu ya nafasi yake katika usimamiaji wa shughuli za madini hasa masoko ya madini yatakapoanzishwa. Hivyo basi niwaombe muwe huru kutoa maoni na kuchangia mijadala itakayokuwa ikiendelea kwani lengo ni kuhakikisha tunapata taarifa na maarifa ya kutusaidia kutimiza wajibu wetu.

Baada ya kusema hayo, napenda kutamka kuwa Warsha hii imefunguliwa rasmi.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki sekta ya madini.

Asanteni sana kwa nisikiliza